KITOVO CHA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU
TAARIFA YA SERA 1| JANUARI 2017

UNIVERSITY of York



# Ustawi, Hatari, na Utendaji wa Haki za Binadamu

Watetezi wa haki za binadamu waliomo hatarini mara nyingi huona ugumu kuzungumzia ustawi wao wa fikira na hisia, hata wanapokuwa na shauku nayo. Tamaduni za utendaji wa haki za binadamu husisitiza kujinyima, ushujaa, na mateso au kifo cha kishahidi. Kanuni hizi huwazuia watetezi kuelezea wasiwasi wao na kutafuta msaada. Tutawezaje kujihusisha na majadiliano kuhusu ustawi katika utendaji wa haki za binadamu? Tutawezaje kuimarisha mbinu za kibinafsi na kijumla za ustawi kati ya watetezi waliomo hatarini?

## Utangulizi

Asilimia 86 ya watetezi wa haki za binadamu waliomo hatarini katika utafiti wetu walielezea kuwa 'kupata kiasi fulani ya shauku' au 'kupata shauku zaidi' kuhusu ustawi wao wa fikira na hisia. Wao walipatwa na shauku katika hili sawa na usalama wao wa kimwili na usalama wa kidijitali.

Katika taarifa hii, tunaelezea maudhui yanayojirudiarudia kuhusu ustawi ambayo yameibuka katika mahojiano na utafiti na watetezi waliomo hatarini kule Kolombia, Meksiko, Misri, Kenya na Indonesia.

### Kurunzi muhimu lakini isiyotosha juu ya ustawi

Hata ingawa watetezi waliomo hatarini wana shauku dhidi ya ustawi wao wa fikra na hisia, hili halijadiliwi mno katika jamii za haki za binadamu. Hata kati ya watetezi wenyewe, hili halitiliwi maanani na kupewa makini

Jinsi ambavyo mtetezi wa Indonesia wa haki za wenye sehemu nyeti za kike na jinsia za kiume alivyosema:

> *Watetezi wa haki za binadamu mara nyingine hukosa kushughulikia [ustawi wao], kwa sababu wao hujishughulisha na kuwasaidia waathiriwa. Hivyo basi, wao mara nyingine husahau kufikiria kuhusu maslahi yao. Mara nyingine, wao hufanya kazi sana na hawana muda wa mapumziko au likizo, na hivyo wanatelekeza ustawi wao wa fikra na hisia.*

Watetezi pia huzipa kipaumbele na umuhimu kazi zao kabla ya kufikiria kuhusu ustawi wao wa kibinfasi. Dhamiri zao imara za kutimiza malengo ya haki za binadamu zinawasukuma mbele pasi na changamoto katika kazi zao.

Mtetezi mwanamke anayefanya kazi ya haki za watu wa LGBTIQ* Kolombia alisema:

> *Shughuli hii ni ngumu. Mara nyingi unapata unyanyapaa. Tunapaswa kujilinda katika mfumo wetu wa jinsia. Ni swali la kujitahidi kuishi. Lakini lazima uendelee na mambo, kufikia kilele, kuanguka mara elfu na kujiamsha kila mara.*

Wanapofikiria kuhusu suala la ustawi, watetezi mara nyingi hulenga ustawi wa waathiriwa wa ukiukaji wa haki za binadamu, kuliko ustawi wao. Watetezi mara nyingine huhisi wenye hatia wakifikiria kuhusu ustawi wao; hisia ni ya anasa.

Mtetezi mwanamke anayefanya katika haki za campesino (wakulima) Kolombia alisema:

> *Hii ni hatua ya mwisho watu huchukua. Tunaanza kwa kuwafikiria watoto wetu, familia zetu, jamii zetu; mtu wa mwisho tunayemfikiria ni sisi. Ni kwa sababu ya 'kupenda sanaa yetu'; hatushughuliki kuwa wahusika wakuu au kutimiza maslahi yetu.*

Hata hivyo, matokeo ya kisaikolojia ya kazi zao zinaweza kuwa kubwa. Watetezi katika utafiti wetu walizungumzia changamoto za kuishi na hofu iliyoenea na wasiwasi; ugumu wao wa kulala; hisia za kukosa nguvu dhidi ya ukandamizaji; kuhisi 'kufa ganzi' au kukosa hisia; kudumu kuwa katika 'hali ya kuhamahama'; na uchovu wao, kukata tamaa, kutengwa, na unyanyapaa.

> *Ninalinganisha kazi yetu na ile ya "Sisyphus": mzigo uliokithiri wa fikira na kimwili bila matokeo dhahiri.... [Tuna] fanya kazi katikati ya vitisho vya mara kwa mara ya kushikwa wakati wowote, na wengine wetu wanashambuliwa katika vyombo vya habari. Kinacholeta ugumu zaidi ni sisi kujua kuwa ikiwa tutaenda kortini, kesi mara kwa mara itakuwa bila haki na yenye mapendeleo na kwamba itakosa uwazi na utaalamu.*
>
> **Wakili wa Haki za Binadamu, Misri**

## Matarajio kuhusu hatari na kujinyima katika kazi ya haki za binadamu

Katika jamii ya haki za binadamu, kuna kanuni imara za kijamii na kitamaduni kuhusu kujinyima, ushujaa, na mateso au kifo cha kishahidi.Hususan katika hali ngumu, hatari zinachukuliwa kuwa yenye asili katika utendaji wa haki za binadamu. Watetezi wanatarajiwa kujinyima na kupambana; wanatarajiwa kukabiliana na kumudu hatari au kuachana na kazi.

Tamaduni ya kuwa shujaa na shinikizo ambazo watetezi huhisi kuhusu kuhitajika (na kuonekana) 'jasiri', huzuia mazungumzo kuhusu ustawi. Katika hali zingine, watetezi wana shauku kuwa kuzungumzia vitisho na mashambulizi walizozipitia na wasiwasi wanazohisi yaweza kukuza hofu na kuwaweka baridi wengine dhidi ya kujiunga na harakati za haki za binadamu.

## Uelewa wa ustawi kutokana na utamaduni

Kati ya watetezi tulipata majibu tofauti kuhusu 'ustawi wa fikira na hisia' katika utafiti wetu. Watetezi wengine walitafsiri hili kama dhana ya mataifa ya 'Magharibi', hivyo kupelekea muingiliano wa 'Magharibi' ambazo haziwafai.

Kiongozi wa jamii ya kiasili ya Kolombiaalisema;

> *Hatutumii dhana ya 'kisaikososiolojia'. Tunaamini kuwa kazi tunayofanya kama watu asili ni yenye manufaa kwetu. Sisi sote tuna akili zetu timamu; sisi sote tuna hisia zetu tano; hatujarukwa akili. Kwa sababu kuna makundi mabaya yalijihami haimanishi kuwa tuko katika hali mbaya.*
>
> *Hata hivyo....kumekuwa na visa 18-20 vya kujiua katika miaka minne iliyopita...Tumejaribu saikolojia ya 'Magharibi', lakini haikusaidia. Madaktari asili wametubariki na kutupa mawaidha. Hili limekuwa bora kwetu.*

Watetezi katika utafiti wetu walitambua kuwa ilikuwa vigumu mara nyingine kuendesha majadiliano kuhusu ustawi na watetezi wenzao kwa sababu ilichukuliwa kuhusishwa na 'uwendawazimu' au kuhitaji daktari wa akili.Waliotambua thamani ya ushauri nasaha na matibabu walitambua ugumu wa kupata aina hizi za msaada pamoja na unyanyapaa unaohusiana na haya. Wengine walihisi kuwa aina za misaada za kitamaduni na kidini za kienyeji zilikuwa za manufaa zaidi kwao.

## Utegemezi wa mbinu za makabiliano ya kibinafsi badala ya kijamii

Watetezi katika utafiti wetu walitegemea mbinu za makabiliano za kibinafsi badala ya msaada wa mashirika katika ustawi wao. Walielezea jinsi ambavyo walipata nguvu kutoka hali yao ya kiroho, katika kuwa na familia na marafiki zao, na katika kujihusisha na shughuli za kuwafurahisha. Hata hivyo, mara nyingine wao hujihisi kupotea na kuwa wapweke katika mapambano yao.

> *Pia hatupati msaada kutoka wenzetu tunapokumbana na shida. Wao hufanya shida yenyewe kuwa 'jambo jepesi'. Kwa mfano, rafiki yangu alipopata barua kutoka kwa polisi kuwa angehojiwa, marafiki wengine walilitilia mzaha, kama, "tulia, tutaenda nawe. Tutakuletea chakula kila siku ikiwa utakamatwa". Tunacheka pamoja. Kupitia niliyoyapitia, natumai, wao pia walihisi hofu. Inaonekana ni kama hatupati msaada wa maadili.*
>
> **Mtetezi dhidi ya ufisadi, Indonesia**

Mashirika ya kijamii machache yameunganisha utendaji wa ustawi katika kazi zao, kwa mfano kupitia kutoa usimamizi katika kazi za kesi; kutoa ushauri nasaha; kuendesha warsha; kusisitiza mizani ya kazi na maisha; na kutoa bima na malipo ya uzeeni.

## Vipengele vya fedha vya ustawi

Watetezi wengi walijadili matatizo ya kifedha ya kazi zao. Walizungumzia utoaji wa fedha wa muda mfupi, mishahara midogo, kutokuwepo kwa manufaa, na matarajio kwamba kazi ya haki za binadamu lazima iendeshwe bila malipo. Watetezi wengine katika utafiti wetu walipoteza mapato kutokana na hatari na vitisho walizozipata. Wengi walilazimika kuchangisha pesa au kutumia akiba zao kwa usalama wa kibinafsi- kama dhamana, matibabu, vifaa vya usalama, na uhamisho. Matatizo ya kifedha yalikuwa magumu zaidi kwa watetezi waliokuwa tayari wakipambana kijamii na kiuchumi.

Mtetezi mwanamke anayefanya kazi katika haki za uzazi na afya ya wajawazito Kenya alisema:

> *Hatuna pesa au mashirika yanayojali haki zetu na familia. Hakuna anayejishughulisha na jinsi ambavyo unakula au kulipa kodi na hakuna shirika ambalo liko tayari kukuajiri kwa sababu huna makaratasi au vyeti vya masaomo...Ni changamoto kwa watetezi wa haki za binadamu, hususan katika ugonjwa au kulazwa hospitalini, tuna watetezi wengi wa haki za binadamu wanaoyapitia haya- fedha ni suala kuu.*

## Kitambulisho, ustawi, na kufikia rasilmali

Kuna uhusiano katika ya kitambulisho cha watetezi, hatari wanazokabiliana nazo, na rasilmali na msaada wanaoweza kupata kwa ajili ya ustawi wao. Watetezi wa LGBTIQ*, kwa mfano, wana nafasi ndogo ya mfumo wa msaada. Kutafuta msaada nje ya jamii yao mara nyingi inawahitaji 'kujitambua' na kuweka hadharani kazi wanayofanya. Hili ni sawa na watetezi wanawake wanaoshughulikia masuala nyeti. Hivyo basi, nafasi zao kazini zinasalia mojawapo ya nafasi chache ya kuimarisha ustawi.


> *[Baada ya mashambulizi] niliamua kuenda nyumbani kwa wazazi wangu; ilikuwa mbaya, unyanyapaa mwingi na ubaguzi kutoka kwa familia yangu. Waliniita mwovu. "Umeangusha jina letu matopeni, tunakuonea aibu, umeangusha jina letu matopeni, huna aibu. Mungu atahakikisha umeenda kuzimu."*
>
> *Ilikuwa ni vigumu sana hadi nikataka kujiua. Sikuweza kuendelea na kazi yangu wakati huo. Kulikuwa na hali ya hofu na hatari kwa LGBTI wote [katika eneo langu]. Nilijificha hadi mambo yalipokuwa salama.*
>
> **Mtetezi wa haki za wenye sehemu nyeti za kike na jinsia za kiume, akijishughulisha na haki za LGBTIQ* Kenya**

## Ustawi kupitia utendaji wa haki za binadamu

Kazi ya haki za binadamu inawaunganisha watetezi kwa njia yenye umuhimu, na kuwaruhusu kupitia kile wanachohisi kuwa muhimu katika ustawi wao. Kwa wengine, kuishi vyema na kuendelea na kazi zao pamoja na vitisho vilikuwa matendo ya uanamapinduzi.

Kwa watetezi hawa, si suala la kuchagua kati ya utendaji wa haki za binadamu na ustawi- bali utendaji wa haki za binadamu unatendwa ili kudumisha ustawi.

> *...makabiliano dhidi ya ukandamizaji yalikuwa mchakato wa uponyaji...kauli kuwa "Ndio, ilikuwa taifa letu" ilikuwa njia yetu ya kuponya jeraha; ni haja ya kihisia na pia kauli ya kutuimarisha, kutufanya tusijihisi wanyonge sana, na pia si wapweke sana. Mapinduzi yetu ni dhidi ya upweke; ni mtandao wa kuaminiana; ni siasa ya mapenzi; mapenzi yanayopotosha...*
>
> **Mwanamke, mwanafunzi na mtetezi wa wanawake, Meksiko**



## Kuunda nafasi za ustawi

Watetezi katika utafiti huu walikaribisha usisitizo zaidi wa kujitunza, kumudu hisia, na majadiliano kuhusu ustawi. Walithamini majadiliano kuhusu jinsi ya kujenga uhusiano na jinsi ya kujenga mbinu za pamoja za ulinzi. Katika mafunzo ya usalama, walithamini kuelezana uzoefu wao katika hatari na hatua zao za ulinzi wao wa kibinafsi pamoja na watetezi wengine; pia walithamini kusikia uzoefu wa wengine.

Walitambua umuhimu wa kuunda nafasi za kujitafakari kuhusu kiasi cha hatari kinachohusiana na kazi zao na kiasi cha kujitolea katika harakati.

*Mtetezi wa haki za binadamu anapaswa kupenda maisha. Kuwasaidia wengine, yeye hawezi kuangukia mtego wa udadisiau kushindwa. Lazima tushinde viwango vyetu vya ndani na nje na hilo litawezekana iwapo tutajitunza. Lazima tusafirishe matumaini na jumbe za kujenga; hatuwezi tukawa na waathirika ili kukuza taabu zaidi. Kwa ujumla, watetezi wa haki za binadamu wana uwezo mkubwa wa kufurahia kila muda wa maisha.*

**Wakili wa Haki za Binadamu, Kolombia**

## Vidokezi kwa Utendaji

Ni muhimu kwa watengenezaji wa sera, weledi, na watetezi wa haki za binadamu:

- Kukuza nafasi za kujitafakari katika ustawi wa kibinafsi na wa pamoja wa watetezi wa haki za binadamu, hususan waliomo hatarini.
- Kutambua na kutatua kanuni na matarajio yanayowapa watetezi ugumu katika kujihusisha na mazungumzo kuhusu ustawi.
- Kupiku mwelekeo wa 'Ulaya' katika kuelewa ustawi. Kutambua, kuhifadhi na kushiriki mbinu zingine za kijamii na kitamaduni za kubuni na kuimarisha ustawi.
- Kukabiliana na ustawi si kama majukumu makuu ya watetezi binafsi bali kama majukumu ya pamoja.
- Kukagua jinsi ambavyo watu, makundi, jamii na washikadau wanaimarisha mbinu za ustawi za kibinafsi na za pamoja. Hizi zinajumuisha kusisitiza utendaji wa utunzaji wa kibinafsi na utunzaji wa wengine; kutia utendaji wa utendaji ndani ya watu pamoja; na kuelewa athari za ufadhili katika harakati endelevu.
- Kutenga fedha katika utendaji wa ustawi ambao ni bora kitamaduni na katika muktadha. Hizi zinaweza kujumuisha utoaji wa matibabu, ushauri nasaha, bima, na malipo ya uzeeni.
- Kutambua kuwa watetezi wengine- kama LGBTIQ* na watetezi wanawake- nafasi kazini ni muhimu kwenye ustawi. Hivyo ni muhimu kuelewa jinsi ambavyo nafasi kazini zinafaa kubadilishwa ili zisiendeleze ukandamizaji, ubaguzi na vurugu, na jinsi ambavyo kuhusishwa, kukubaliwa na kujumuishwa kunaweza kuimarishwa katika jamii ya haki za binadamu.

**Kuhusu Mradi huu:**

Taarifa ya Sera hii inatokana na matokeo ya utafiti ya mradi 'Kuepuka Hatari, Kumudu Usalama, na Kupokea Msaada' ambao unachunguza uzoefu wa watetezi wa haki za binadamu waliomo hatarini Kolombia, Meksiko, Misri, Kenya, na Indonesia.

Mahojiano na tafiti zilifanyika na zaidi ya watetezi wa haki za binadamu 400 kati ya Julai 2015 na Novemba 2016.

Centre for Applied Human Rights
University of York
Yorkshire House
6 Innovation Close, York Science Park
Heslington, York YO10 5ZF
United Kingdom

+44 (0)1904 325830
cahr-admin@york.ac.uk
***york.ac.uk/cahr***

**Mtafiti Mkuu:**
Alice M. Nah

**Timu ya utafiti**
Sherif Azer
Patricia Bartley
Peter Cousins
Indria Fernida
Kholoud Hafez
Budi Hernawan
Irina Ichim
Katrina Maliamauv
Erick Monterrosas
Patrick Mutahi
Paola Pacheco Ruiz
Emily Schmitz

**Kwa taarifa zaidi**
***securityofdefendersproject.org***
security-of-defenders-project@york.ac.uk

**Marejeo**
Nah, A.M. (2017) Wellbeing, Risk, and Human Rights Practice, Human Rights Defender Hub Policy Brief 1, Centre for Applied Human Rights, University of York: York, available at ***securityofdefendersproject.org***

**Mchoraji**
Lara Luna Bartley

**Kubuni**
Design and Print Solutions

34382 – york.ac.uk/design-print-solutions